



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TAARIFA KWA UMMA**  
**KUHUSU UTEUZI WA MBUNGE WA VITI MAALUM**

Dar es Salaam 03 Novemba, 2023

Katika kikao chake leo tarehe 03 Novemba, 2023, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia matakwa ya ibara ya 78(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 86A (6) na (8) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, imemteua Ndugu **AZIZA SLEYUM ALLY** kuwa Mbunge wa Viti Maalum wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Uteuzi huo umefanyika baada ya Tume kupokea barua yenye Kumb. Na. CEA.137/400/02A/22 ya tarehe 19 Agosti, 2023 kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyoandikwa kwa mujibu wa kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 ikiitarifu Tume kuhusu uwepo wa nafasi wazi ya Ubunge wa Viti Maalum wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kufuatia kujiuzulu aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum **Mhe. Bahati Keneth Ndingo**.

Imetolewa na:-

Kailima, R. K.

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**